THE NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA

# EXAMINERS' REPORT ON THE PERFORMANCE OF CANDIDATES CSEE, 2012

# 021 KISWAHILI
## (School Candidates)

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TATHMINI YA WATAHINI KUHUSU UFAULU WA WATAHINIWA WA KIDATO CHA NNE, 2012

# SOMO LA KISWAHILI

Kimechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624, Dar es Salaam, Tanzania

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2013

Haki zote zimehifadhiwa

## YALIYOMO


Dibaji……………………………………………………………………………iv

1.0 Utangulizi……………………………………………………………1

2.0 Tathmini kwa kila Swali……………………………………………..1

2.1 Sehemu A: Ufahamu……………………………………………………1
- 2.1.1 Swali la 1: Ufahamu……………………………………...................1
- 2.1.2 Swali la 2:Ufupisho………………………………...……..…....5

2.2 Sehemu B: Sarufi na Utumizi wa Lugha…………………………..…………9
- 2.2.1 Swali la 3: Sarufi………………………………………………..………7
- 2.2.2 Swali la 4: Sarufi……………………………………………………..10
- 2.2.3 Swali la 5: Utumizi wa Lugha…………………………………………..11
- 2.2.4 Swali la 6: Sarufi……………………………………………….……13
- 2.2.5: Swali la 7: Sarufi……………………………………………..……15

2.3 Sehemu C: Uandishi…………………………………………………..…...17
- 2.3.1 Swali la 8: Uandishi wa Insha…………………………………..…....17
- 2.3.2 Swali la 9: Uandishi wa Kumbukumbu za Mkutano………………..……..19

2.4 Sehemu D: Maendeleo ya Kiswahili……………………………………..…..22
- 2.4.1 Swali la 10: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili……………....................22

2.5 Sehemu E: Fasihi kwa Ujumla………………………………………..……...25
- 2.5.1 Swali la 11: Methali………………………………..……………...25
- 2.5.2 Swali la 12: Ushairi………………………………........................29
- 2.5.3 Swali la 13: Riwaya………………………………..…………...32
- 2.5.4 Swali la 14: Tamthiliya…………………………………….……...38
- 2.5.5 Swali la 15: Fasihi Simulizi………...……………………….………43

3.0 Hitimisho……………………………………………………….…....48

3.1 Mapendekezo………………………….............................................48

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linayo furaha kutoa taarifa ya watahini kuhusu ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuhitimu Kidato cha Nne kwa somo la Kiswahili. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu katika mitihani kwa wanafunzi, walimu, wazazi waandaaji wa sera na jamii kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa kipi mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa wawapo katika elimu ya Sekondari.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vibaya au vizuri katika mtihani wao. Taarifa inaonesha baadhi ya sababu zinazofanya watahiniwa kutopata alama za juu katika majibu yao. Sababu hizo ni kama vile kutoelewa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa watahiniwa kujieleza kwa ufasaha na udhaifu katika kuelewa dhana zinazohusiana na somo la Kiswahili. Mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa shule, walimu na wanafunzi kupata mbinu muafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo inayooendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania litapenda kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na umma kwa ujumla ambayo yatatumika katika kuboresha taarifa za watahini zitakazofuata. Kila shule itapewa nakala moja ya ripoti kwa upendeleo. Nakala za ziada zinaweza kununuliwa kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania. Taarifa kuhusu bei na gharama za posta zinaweza kutolewa na Baraza pale shule itakapohitaji.

Mwisho Baraza linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, walimu wa somo na wengine wote waliohusika katika kutayarisha taarifa hii. Tunapenda vilevile kutoa shukrani zetu za pekee kwa wafanyakazi wa Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano walioshiriki katika uchambuzi wa data zilizotumika katika ripoti hii.

Dr. Charles E. Msonde

**KAIMU KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua ufaulu wa watahiniwa wa mtihani wa Kidato cha nne wa mwaka 2012 kwa somo la Kiswahili. Mtihani ulikuwa na maswali 15 yaliyogawanywa katika sehemu A, B, C, D na E. Katika sehemu A, B na D watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote, sehemu C ilikuwa na maswali (2) ambapo mtahiniwa alipaswa kujibu swali moja (1) tu. Sehemu E ilikuwa na maswali **matano** (**5**) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu (3) na swali la 15 lilikuwa la lazima.

Mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2012 ulifanywa na watahiniwa **396,975** kati ya watahiniwa hao, waliofaulu ni **189,230** sawa na asilimia **51.05** ya watahiniwa wote waliofanya mtihani, yaani waliopata daraja A hadi D na waliopata daraja F ni asilimia **48.95**. Kiwango hicho cha ujumla cha ufaulu kilikuwa cha kuridhisha kiasi ukilinganisha na kilivyokuwa mwaka 2011, kwani wastani wa alama za watahiniwa kwa mwaka 2011 ulikuwa **21.6** kati ya alama 100 wakati wastani kwa mwaka 2012 ulikuwa **25.12** kati ya alama 100. Aidha asilimia ya waliofaulu kwa mwaka 2011 ilikuwa **37.08** ambayo ni ya chini kuliko asilimia ya waliofaulu 2012.

Taarifa hii inaelezea uchambuzi wa maswali ya mtihani na majibu yaliyotolewa na watahiniwa. Sampuli za majibu ya watahiniwa pia zimewekwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kile kilichofanywa na watahiniwa. Uchambuzi huu unatarajiwa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi walioko shuleni.

# 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

Uchambuzi umefanyika kwa kuyapitia maswali kumi na tano ya karatasi ya mtihani wa Kiswahili kwa kuangalia sampuli ya majibu ya watahiniwa. Idadi ya watahiniwa kwa asilimia waliofanya mtihani, kwa kila swali imeoneshwa pia.

## 2.1 Sehemu A: Ufahamu

### *2.1.1 Swali la 1: Ufahamu*

Swali la kwanza lilihusu mada ya Ufahamu na lilikuwa na vipengele vinne vya maswali vilivyobeba jumla ya alama 5. Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari alichopewa na kisha kujibu maswali yanayofuata kutokana na kifungu hicho. Sehemu (a) ya swali ilimtaka mtahiniwa kufafanua maana za misemo kama ilivyotumika katika habari aliyosoma.

(i) Nzi kufa kwenye kidonda si hasara
(ii) Kila mtu akashughulika na hamsini zake

(iii) Ushikwapo shikamana na
(iv) Siku za mwizi arobaini

Kipengele hiki cha (a) kilikuwa na jumla ya alama 2, kwa kila ufafanuzi wa msemo ukiwa umebeba alama 00$^1/_2$. Sehemu (b) mtahiniwa alitakiwa kueleza sababu za uongozi wa shule kupiga vita tabia ya wanafunzi kusoma wakati wa usiku wa manane, sehemu (c) alitakiwa kutoa mawazo yake kuhusu kitendo cha Tatu kufuatilia mienendo ya wanafunzi wenzake kusoma usiku wa manane, na sehemu (d) alitakiwa kuandika kichwa cha habari kisichozidi maneno matano (5). Kwa kila kipengele cha b-d kilipewa alama moja (1).

Swali hili lilijibiwa na asilimia 87.9 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani ambapo watahiniwa waliopata alama 0 ni asilimia 20. Watahiniwa hawa walishindwa hata kuandika kichwa cha habari. Kwa mfano, waliandika Siku za mwizi, Ushikwapo shikamana, Siku za mwizi ni arobaini, hivyo kushindwa kabisa kuandika kichwa cha habari ilivyopasa. Aidha watahiniwa hao walishindwa kabisa kufafanua maana za misemo kama ilivyotumika katika habari. Katika vipengele vya (b) na (c) watahiniwa hao walishindwa kabisa kutoa majibu sahihi. Hivyo watahiniwa hao walipata alama 0 kwani walishindwa kuhusisha yale maovu yanayofanyika nyakati za usiku na majukumu ya Tatu kama Kiongozi kama sababu iliyofanya uongozi kupiga vita tabia ya kusoma usiku na Tatu kufuatilia mienendo ya wanafunzi wenzake, badala yake wakatoa sababu wanazozifikiria wao bila kuhusisha na habari, kwa mfano waliandika, " *kwa sababu walijua kila mtu amelala na kuwa hayupo mwalimu wa zamu*." Kielelezo 1.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa ambaye hakukidhi matakwa ya swali.

**Kielelezo 1.1**



1. Mzi kufa kwenye kidonda si hasara maana mewe ambaye hufanyagi ma kosa utakamatwa na wle ambaye amezoea hatakamatwa.

ii Kila mtu akishughulika na hansini zake maana yake. Kila mtu atawuna alicho kipanda.

iii Ushikwapo shikamana ~~maan~~ maana yake hakuna siri cha watu wawili

iv Siku za mwizi ni arobaini maana yake wale ambao ~~wanatorokaga~~ ka wanatorokaga walikamatika ndivyo ilivyo tumika katika habari.

bi Kwa sababu ilikuwa saa nane za usiku tukaingia katika chumba cha ~~kuonyesha~~ kuonesha picha, tuka funga mlango kwa funguo na komeo

c Ni ile hali ya kufunga mwanafunzi mwenzao wao wameenda kuangalia vichekecho

d. Kichwa cha habari ni SHULE ~~HATI~~ WANAFUNZI KUSOMA

Kielelezo 1.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi kulingana na kifungu cha habari alichopewa.

Asilimia 5.7 ya watahiniwa waliopata alama 3 – 5 waliweza kutoa ufafanuzi wa misemo kama ilivyotumika katika kifungu cha habari walichopewa, kutoa sababu za uongozi wa shule kupiga vita usomaji wa usiku wa manane, kutoa mawazo yao kuhusu kitendo cha dada mkuu Tatu kufuatilia mienendo ya

wanafunzi wenzake na kuandika kichwa cha habari kulingana na matakwa ya swali. Kielelezo kifuatacho ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kutokana na matakwa ya swali.

**Kielelezo 1.2**

SEHEMU-A

1. (a) (i) Nzi kufa kwenye kidonda si hasara, una maana kwamba mtu akipewa adhabu kwa sababu ya jambo ambalo amefanya kwa manufaa yake haitomuuma.

(ii) Kila mtu akashughulika na hamsini zake, maana yake kila mtu akaendelea na kufanya mambo yake.

(iii) Ushikwapo shikamana, ina maana pale unapopatwa na jambo gumu, upatapo njia ndogo usisite kuifuata maana unaweza ukaokoka.

(iv) Siku za mwizi arobaini, ina maana kuwa hata iweje ufanyapo makosa, ipo siku ya kukamatwa.

(b) Kwa sababu uongozi wa shule unafikiri huo unaweza ukawa mwanya wa wanafunzi kutoroka shuleni.

(c) Tatu ni dada mkuu wa shule hivyo ni jukumu lake kuhakikisha kuwa wanafunzi wenzake wanafuata sheria za shule ikiwemo kutosoma usiku.

(d) MAISHA YA SHULE

Kielelezo 1.2 ni sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa aliyetoa majibu yaliyofafanua vizuri kifungu hicho cha habari.

### 2.1.2 *Swali la 2: Ufupisho*

Swali hili lilihusu mada ya Ufahamu, kipengele cha ufupisho. Swali lililenga kupima stadi ya Ufahamu, Maarifa na Uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari alichopewa kisha kufupisha habari hiyo kwa maneno 40. Swali hilo lilikuwa na jumla ya alama tano (5) na lilijibiwa na asilimia 80.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Watahiniwa wengi yaani asilimia 83.0 walipata chini ya alama 2.5 ambapo miongoni mwao asilimia 25.5 walipata alama 0. Watahiniwa hao walikuwa na upungufu katika majibu yao kwa kuwa: walipotosha kiini cha habari ya awali, hawakuzingatia taratibu za uandishi, hawakuzingatia matumizi ya lugha sanifu, hawakuzingatia idadi ya maneno na hawakuzingatia mtiririko wa mawazo wenye mantiki. Kwa mfano baadhi ya watahiniwa hao walishindwa kabisa kuzingatia kanuni za ufupisho, kutoelewa maana ya ufupisho wa habari kama kielelezo 2:1 kinavyoonesha.

**Kielelezo 2.1**

2 Somo Kifungu cha habari Kisha

Kifungu cha habari

Tuli Kuwa Katika body - shule ya Kulipia
Mimi na Wanafunzi wenzangu tuli Kuwa tuna
pendelea Sana Kuchera Mpira hata Kushabi
Kia huo Mpira

Lakini walimu wetu husussa Mwalimu wa
taaluma ali Kuwa apende Kutuona tuKisha
shabiKia Mpira Kwa Sababu sisi wanafunzi
Na Mwanafunzi tusipendelee Sana hushabiKi
Wa Mpira tuwe bizena na Masomo

Wanawafunzi wengi

Kielezo 2.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye hakuweza kukidhi matakwa ya swali. Mtahiniwa huyu anazungumzia ushabiki wa mpira ambao hauhusiani kabisa na habari ya awali iliyomtaka aifupishe. Aidha amechanganya

lugha ya kiingereza katika majibu yake mfano ametumia neno “body”. Pia hakuzingatia lugha sanifu mfano neno “bize”.

Mtahiniwa mwingine katika kujibu swali la 2 aliandika ufupisho wake kama hivi, “*Vijana wanampe kutembea usiku kucha pengine hata kujikwaa kisiki kisha vigana hukiuka na kukiangalia kisiki hicho ambacho pengine huwa hakitazamiki.*

*Kama kisiki kimkwazavyo mtu atembeaye usiku pia mikasa mbalimba midogo kwa mikubwa huwakwaza na pigine hata kubwaga chini binadamu.*’’

Mtahiniwa huyu aliandika habari ambayo haihusiani kabisa na habari ya awali. Aidha ametumia maneno yasiyo sanifu kama ‘ pegine’ “wanampe”, “vigana” na “mbalimba” ambayo yaliifanya habari hii kutokuwa na mtiririko wenye mantiki. Watahiniwa wachache sana (2%) waliweza kuzingatia taratibu za uandishi kwa kupanga mawazo kwa mtiririko wenye mantiki na walizingatia idadi ya maneno. Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyezingatia taratibu hizo.

## Kielelezo 2.2


2. Imeundwa kamati maalum ya kuandika upya historia ya Bara la Afrika. Mpango huu unaungwa mkono na wananchi kwani utatokomeza maandishi yaliyoandikwa na wakoloni waliopotosha ukweli. Mpaka leo ni watu wachache ~~wanaoamini~~ wanaopenda utamaduni wao. Ni imani kwamba baada ya miaka michache hali itabadilika.

Kielelezo 2.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutumia maneno yake mwenyewe bila kupotosha kiini, alizingatia mtiririko wa mawazo wenye mantiki, taratibu za uandishi na matumizi ya lugha sanifu. Aidha mtahiniwa huyu hakuzingatia idadi ya maneno yanayotakiwa katika kifungu hicho cha habari, hivyo kutokupata alama zote.

## 2.2 Sehemu B: Sarufi na Utumizi wa Lugha

### *2.2.1 Swali la 3: Sarufi*

Swali lilitoka katika mada ya sarufi na lililenga kupima maarifa, uundaji pamoja na kumbukumbu ya yale aliyojifunza. Aidha swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua kwa kutumia mifano dhahiri kuhusu dhana alizopewa. Swali lilikuwa na jumla ya alama tano (5).

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wengi ambao ni asilimia 83.8, kati yao asilimia 67.6 walipata kati ya alama 0 hadi 1.5 na asilimia 35.3 walipata alama 0. Watahiniwa hawa walikuwa na upungufu katika majibu yao kwani walishindwa kabisa kufafanua dhana na kuzitolea mifano dhahiri katika vipengele vyote vilivyotolewa. Kwa mfano mtahiniwa mmoja katika jibu lake ambalo halikukidhi matakwa ya swali katika kipengele (a) hadi (e) aliandika kama ifuatavyo:

(a) "*Kiima ni hali ambayo kutoa maana*"(b) "*Chagizo ni hali ambayo mtuuwenza kumsaidia kuanzisha chagizo fulani au kiasi*
(d) "*Utohoaji ni ile hali ambayo unaweza kuzalisha kitu kingine kutumia neno utohoaji* (e) *"urudifishaji ni hali ambayo ya kula vyakula vya rudumba na kwenda kurudubishwa tumboni wa mtu au kiumbe kinginecho."*\

Licha ya mtahiniwa kutoa majibu yanayokinzana na kutumia maneno ya lugha za asili kama neno *"rudumba"*, mtahiniwa huyu ana matatizo ya kisarufi kwa kuandika neno *"kurudubishwa"* badala ya "*kurutubishwa.*"

Hata hivyo, asilimia 17.2 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata kati ya alama 2.5 na 5. Watahiniwa hao waliweza kufafanua dhana mbalimbali walizopewa na kutoa mifano. Kwa mfano katika kielelezo 3.1 mtahiniwa alijibu kwa kufuata matakwa ya swali.

**Kielelezo 3.1**

3 a) Kiima, ni sehemu ya sentensi ambayo huta-ja mtenda au mtendwa wa jambo. Mfano;
- Baba / analima shamba
K

b) Chagizo, ni sehemu ya sentensi ambayo hujazwa na kielezi cha aina yoyote upande wa kiarifu. Mfano
- Juma anaenda shuleni
Ch

c) Shamirisho, ni sehemu ya sentensi ambayo hukaliwa au kujazwa na kivumishi, kiwakilishi na nomino ya aina yoyote upande wa kiarifu.
Mfano;
- Mama analima shamba
Sh

d) Utohoaji, ni kitendo cha kuchukua maneno au misamiati toka lugha moja na kuipeleka katika lugha nyingine.
Mfano: kutoka lugha ya kiingereza kwenda kiswahili. Kama
Shirt — shati.

e) Uradidishaji, ni kitendo cha kurudiarudia maneno Mfano;
Motomoto, hodihodi, harakaharaka.

Kielelezo 3.1 kinaonesha jinsi mtahiniwa alivyoweza kueleza na kufafanua kwa kutumia mifano dhahiri dhana alizopewa.

### *2.2.2* Swali la 4: Sarufi

Swali hili lilitoka katika mada ya aina za maneno na lililenga kupima matumizi, ujuzi na maarifa ya mtahiniwa. Swali lilimtaka mtahiniwa kubadili aina za maneno aliyopewa kwa kufuata maelekezo yaliyo kwenye mabano kama ifuatavyo:

(a) Mkono (badili kuwa kielezi)
(b) Kwenda (badili kuwa nomino)
(c) Bora (badili kuwa kitenzi)
(d) Ogopa (badili kuwa kivumishi)
(e) Mzazi (badili kuwa kitenzi)
(f) Bisha (badili kuwa kivumishi)
(g) Refu (badili kuwa kitenzi)
(h) Linda (badili kuwa nomino)
(i) Kabati (badili kuwa kielezi)
(j) Uguza (badili kuwa nomino)

Swali hili lilikuwa na jumla ya alama tano (5).

Watahiniwa wengi (asilimia 87.4) kati ya waliofanya mtihani walijibu swali hili. Asilimia 45 waliweza kujibu swali hili na kuweza kupata kati ya alama 2 hadi 5. Aidha asilimia 23.8 walishindwa kabisa kuelewa matakwa ya swali kutokana na kutokufahamu vizuri aina za maneno. Baadhi ya watahiniwa hao walinyumbua maneno badala ya kuyabadili ili kupata aina nyingine za maneno. Watahiniwa wengine walitunga sentensi zisizoeleweka kwa kutumia maneno hayo. Kielelezo 4.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye sentensi zake hazikuwa na mantiki.

**Kielelezo 4.1**


4(a) mkono
ni kufanya kitu na mwenzako kwa umo
ja hata wingi ~~tut~~ kufurahi kwa pamoja
~~et~~ ndo ile hali ya kuse kwamba tume
muunga mkono katika sherehe yake ya
maafali

(c) Bora
nikufanya kitu kwa kusema bora
ningefanya kitufulani kingenisaidia ~~ba~~
baadae

Kielelezo 4.1 kinaonesha mtahiniwa aliyeshindwa kutumia maneno aliyopewa kama ilivyoelekezwa, hivyo akatunga sentensi ambazo hazikuwa na mantiki.

Aidha, watahiniwa wengine hawakufuata matakwa ya swali na usanifu wa lugha hivyo kujibu tofauti na maelekezo kama mfano ufuatao unavyoonesha:,

*(a) Mkono - Mkononi*

*(b) Kwenda – Konda*

*(c) Bora- ubora*

*(d) Ogopa – ogopesha*

*(e) Mzazi - Kizazi*

*(f) Bisha- ubishi*

(g) *Refu – urefu*

*(h) Linda – windo*

Mtahiniwa huyu hakufuata maelekezo kuanzia kipengele (b) – (h) kwani katika kipengele (b) neno *Konda* sio sanifu kuwa nomino, (c) *ubora* sio kitenzi bali ni nomino, (d) *ogopesha* sio kivumishi bali ni kitenzi (e) *Kizazi* sio kitenzi bali ni nomino, (f) *Ubishi* sio kivumishi bali ni nomino, (g) *Urefu* sio kitenzi bali ni nomino na (h) *Windo* ni nomino inayotokana na neno winda na sio linda.

Watahiniwa wachache yaani asilimia 3.9 tu walijibu swali hili kwa kuzingatia haja ya swali na kupata kati ya alama 4 hadi 5. Kielelezo 4.2 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa kufuata matakwa ya swali.

**Kielelezo 4.2**


4.
(a) Mkono - mkononi
(b) Kwenda - mwendo
(c) Bora - Boresha
(d) Ogopa - Mwoga.
(e) Mzazi - Zaa
(f) Bisha - Mbishi
(g) Refu - Refuka, Refusha
(h) Linda - Lindo
i) kabati - kabatini
j) Uguza - Muuguzi

Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kubadili aina za maneno waliyopewa kwa kwa kufuata maelekezo yaliyokuwepo kwenye mabano na hivyo kupata alama zote 5.

### *2.2.3 Swali la 5: Utumizi wa Lugha*

Swali lilitoka katika mada ya utumizi wa lugha na lililenga kupima ujuzi, maarifa na matumizi ya kamusi kwa mtumiaji wa lugha. Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja hoja tano zinazothibitisha umuhimu wa kamusi kwa mtumiaji wa lugha. Swali lilikuwa na alama 5. Asilimia 86.0 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili, miongoni mwao asilimia 70.5 walipata chini ya alama 2.5 ambapo kati yao asilimia 20.8 walipata alama 0. Baadhi ya watahiniwa hawa walieleza kuhusu lugha badala ya umuhimu wa kamusi. Aidha, watahiniwa wengine hawakuelewa ipasavyo matakwa ya swali hivyo kutaja mambo yasiyohusiana na umuhimu wa kamusi kama vile *kauli mbalimbali za maneno, kufahamisha maneno mapya, kufahamisha maneno ya lugha za kigeni, hutoa tafsiri ya misamiati ya Kiswahili* na *huhifadhi kumbukumbu ya misamiati iliyosanifiwa.* Mtahiniwa aliyetoa majibu hayo alishindwa kutofautisha kati ya sifa za kamusi na umuhimu wa kamusi. Kielelezo 5.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa yasiyofuata matakwa ya swali.

**Kielelezo 5.1**


5. Kamusi ni muhimu kwa mtumiaji yeyote wa lugha. Taja hoja tano zinazothibitisha umuhimu huo.
i. Kukuza lugha ya Kiswahili
ii. Kuongeza msamiati katika lugha
iii. Kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili
iv. Kuburudisha jamii kwa ujumla
v. Kukamilisha na kuongeza ujuzi katika Kiswahili

Kielelezo 5.1 kinaonesha mtahiniwa aliyeshindwa kueleza umuhimu wa kamusi na kujikita kueleza mambo yasiyohusiana na umuhimu wa kamusi kwa mfano katika kipengele cha (iv) mtahiniwa ameandika kuwa umuhimu wa kamusi ni "kuburudisha jamii kwa ujumla."

Asilimia 4.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili waliweza kutaja kwa usahihi hoja nne hadi tano zilizothibitisha umuhimu wa kamusi kwa mtumiaji wa lugha. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 5.2**


5. Hoja tano zinazothibitisha umuhimu wa Kamusi.
(i) Kamusi inatusaidia kujua maana za maneno. Maneno yanaweza kuwa ya lugha moja au lugha tofauti.
(ii) Kamusi inatusaidia kujua matumizi ya maneno mbalimbali
(iii) Kamusi inatusaidia kujua aina za maneno kama vile; nomino, kivumishi au kitenzi.
(iv) Kamusi huonyesha matamshi ya maneno mbalimbali. Kwa hivyo inatusaidia kutoa matamshi sahihi ya maneno mfano thelathini badala ya selasini.
(v) Kamusi huonyesha asili ya neno

Kielelezo 5.2 kinaonesha mtahiniwa aliyeweza kutaja hoja tano na kutoa mifano katika baadhi ya hoja ili kudhihirisha usahihi wa hoja alizozitoa.

### *2.2.4 Swali la 6: Utumizi wa Lugha*

Swali hili limetoka katika mada ya matumizi ya lugha na lilimtaka mtahiniwa kutumia mifano ya lugha ya Kiswahili ili kutaja sababu tano za utata katika mawasiliano. Aidha, ilitakiwa mifano ioneshe maana mbili au zaidi ili kuonesha utata huo. Swali lilikuwa na jumla ya alama tano (5).

Swali hili lilijibiwa na asilimia 77.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani, ambapo asilimia 93.9 walishindwa kujibu swali kwa usahihi hivyo kupata chini ya alama 2. Aidha asilimia 61.7 walipata alama 0. Watahiniwa hao walishindwa kabisa kutumia mifano ya lugha ya Kiswahili kutaja sababu tano za utata katika mawasiliano. Kielelezo 6.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambayo hayakukidhi matakwa ya swali.

**Kielelezo 6.1**


6i/ Television
ii/ Magazeti
iii/ Radio
iv/ Simu za mkononi
v/ Njia ya uchukuzi

Kielelezo 6.1 kinaonesha mtahiniwa ambaye ametaja vyombo vya habari na njia za mawasiliano kama vile simu za mkononi, magazeti na redio badala ya kuzingatia maana na unyambuaji wa maneno, taratibu za uandishi, mkazo wa sauti na muktadha wa matumizi ya neno kama ilivyotakiwa.

Aidha ni asilimia 1.4 tu ya watahiniwa waliofanya mtihani ndiyo walioweza kueleza hoja tano vizuri kudhihirisha utata uliopo. Kielelezo 6.2 kinaonesha watahiniwa waliokidhi haja ya swali kwa kutaja sababu tano za utata katika mawasiliano.

**Kielelezo 6.2**

6. Sababu za utata ni;-

(i) Kutumia neno lenye maana zaidi ya moja.
Mfano: Amenunua mbuzi.
-Sentensi hii yaweza kumaanisha amenunua mbuzi mnyama au kifaa cha kukunia nazi.

(ii) Kutumia maneno yenye maana ya picha.
Mfano: Nimeacha ua langu nyumbani.
Neno ua laweza kuwa mmea au mzunguko mzuri

(iii) Kutotumia mkazo wa sauti wakati wa kuzungumza.
Mfano: neno 'barabara' likitiliwa mkazo kumaanisha 'haswa haswa' lakini likipotiliwa mkazo humaanisha 'njia' ya kupitia magari, watu na wanyama.

(iv) Kutozingatia kanuni (alama) za uandishi
Mfano
Baba Juma amerudi jana.

-Sentensi hii yaweza kuwa na maana ya kuwa Baba Juma alifika jana. au Baba anaambiwa kuwa Juma alifika jana.

(v) Kutozingatia mazingira na muktadha.
Mfano: Simba ameuawa.
Hii yaweza kuwa mnyama au mtu aitwaye Simba ameuawa.

Kielelezo 6.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kulingana na matakwa ya swali. Mtahiniwa huyu ameweza kueleza sababu tano za utata uliopo katika lugha na kutoa mifano inayodhihirisha utata huo.

### 2.2.5 *Swali la 7: Utumizi wa Lugha*

Swali lilihusu utumizi wa lugha. Swali lilitoka katika mada ya mjengo wa tungo. Swali lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa kuhusu muundo wa kirai nomino katika tungo. Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja miundo mitano ya kirai nomino kwa kutoa mfano kwa kila muundo na lilikuwa na jumla ya alama 5.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 56 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani ambapo miongoni mwao asilimia 91.6 walipata chini ya alama 2.5 na kati yao asilimia 74.4 walipata alama 0. Watahiniwa hawa walishindwa kabisa kutaja miundo ya kirai nomino badala yake walitoa majibu ambayo yako nje kabisa ya matakwa ya swali. Mfano majibu ya mtahiniwa mmoja aliandika, "*Nomino, Kitenzi, Kivumishi, Kielezi, Kiwakilishi*" kama miundo wakati ni aina za maneno. Mtahiniwa mwingine aliandika. "

*(i) Haina kitenzi ndani yake. Mfano Mtoto aliyekuja jana*
*(ii) Hutoa taarifa isiyo kamili. Mfano Anayeumwa*
*(iii) Hutegemea kishazi huru ili kufikisha ujumbe. Mfano Juma anacheza mpira uwanjani'*

Mtahiniwa huyu hajaonesha muundo wowote wa kirai nomino, badala yake alitoa maelezo kuhusu sifa ya kirai nomino na hata mifano aliyotoa haiendani na maelezo yake. Kielelezo 7.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambayo hayakukidhi haja ya swali.

**Kielelezo 7.1**


7. i Kirai nomino
i) Sentensi
ii) muundo
iii) Kishazi tegemezi
iv) Kishazi huru
v) Sarufi

Kielelezo 7.1 kinaonesha mtahiniwa ambaye ametoa majibu yaliyo nje kabisa ya matakwa ya swali. Mtahiniwa huyu badala ya kutaja miundo ya kirai nomino ameorodhesha dhana nyingine tofauti kabisa, mfano ametaja sentensi, muundo, sarufi ambavyo havihusiani na matakwa ya swali.

Asilimia 3.6 ya watahiniwa waliweza kutaja miundo ya kirai nomino kwa usahihi na kutoa mifano sahihi kwa kila muundo wa kirai nomino. Pia mpangilio wa kazi zao ulikuwa mzuri na ulio wazi. Aidha, watahiniwa waliopata alama zote waliweza kutaja miundo na mifano ya kirai nomino na kuweka kipashio "KN", pia walitoa mifano sahihi kwa kila muundo. Kielelezo 7.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo7.2**



7\. i) Kirai nomino inamiundo mifano:-

i) Nomino ikisimama peke yake.

mfano: Mama/ anapika vizuri.
KN

ii) Nomino na nomino katika sentensi.

mfano: Baba na Mama/ wanakula.
KN.

iii) Nomino na kivumishi katika sentensi

mfano: Mtoto yule/ ni mjanja.
KN

iv) Kiwakilishi katika sentensi (Pekee yake).

mfano: Mimi / ni mwanafunzi.
KN.

7\. v) Kivumishi na Nomino katika sentensi.

mfano: Yule mtoto ni mtundu sana.
KN

Kielelezo 7.2 kinaonesha mtahiniwa aliyelielewa swali vizuri na kulijibu kama linavyotakiwa kwa usahihi isipokuwa katika mfano wa (v) amekosea muundo uliojenga kirai nomino kwani umejengwa na kiwakilishi na nomino na sio kivumishi.

## 2.3 Sehemu C: Uandishi

### *2.3.1 Swali la 8: Uandishi wa Barua ya Kirafiki*

Swali la 8 lilihusu mada ya utungaji katika kipengele cha uandishi wa barua. Swali lililenga kupima utumizi na maarifa ya kuandika barua ya kirafiki. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika barua ya kirafiki ili kutoa taarifa ya kutohudhuria sherehe aliyoalikwa. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 10. Asilimia 59.3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili ambapo miongoni mwao asilimia 52.5 walipata kati ya alama 06 hadi 10. Kielelezo 8.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa kufuata matakwa ya swali.

**Kielelezo 8.1**

8.

SHULE YA SEKONDARI MATATIZO,
S.L.P 10001,
KIZINGITI.
09 - 10 - 2012.

Mpendwa rafiki,

Kwanza ningependa kukushukuru sana kwa barua yamwaliko na pia ninatanguliza salamu zangu za dhati kwako pamoja na familia ya Mzee Matata.

Natanguliza samahani kabla ya kuendelea kwani kwa wakati huo sitaweza kuhudhuria sherehe hiyo kutokana na muingiliano wa majukumu. Nasema haya kwa sababu mnamo tarehe 7 mwezi wa 10 mwaka huu nitakuwa safarini kikazi kuelekea mkoani Singida ambako nitazuru shule mbalimbali kuangalia mazingira ya kufundishia kwa muda wa siku saba.

Napenda tena kusema shukrani na samahani kwa kutoweza kuhudhuria. Naomba wapo salamu wote watakao-hudhuria pamoja na Mzee Matata.

Wako,

Tumaini Baraka.

Kielelezo 8.1 kinaonesha mtahiniwa aliyeweza kuzingatia vipengele vyote vya muundo wa barua ya kirafiki. Hata hivyo mtahiniwa huyu alishindwa kutaja jina la rafiki yake “Faraja Matata” aliyemwandikia barua.

Hata hivyo, asilimia 14.4 ya watahiniwa waliofanya mtihani walipata alama 0 kwani hawakuzingatia matakwa ya swali. Baadhi yao waliandika barua za kikazi badala ya kirafiki na wengine walinakili sehemu ya swali kama jibu la swali hilo. Kielelezo 8.2 na 8.3 ni mifano inayodhihirisha hilo.

**Kielelezo 8.2**



8:

Tumaini Baraka,
SLP 109,
BUKOBA.

09/10/2012.

Faraja Matata,
SLP 109,
BUKOBA.

Ndugu,

YAH: KUTOKUHUDHURIA SHEREHE YAKO YA KUZALIWA.

Kichwa cha habari hapo juu cha husika.
Ninaitwa Tumaini Baraka. Kwanza kabisa ninashukuru kupata mwaliko wako lakini sitaweza kuhudhuria sherehe hiyo kwasababu ifuatayo. Siku ~~tatu~~ tatu kabla ya sherehe yako ninasafari ya kuelekea Singida. Hivyo naomba unisamehe.
Sitaweza kuwa nanyi kimwili lakini tutakuwa sote kiroho.

Wako rafiki,
Tumaini Baraka
T. Baraka
rafiki.

Kielelezo 8.3 kinaonesha muundo wa barua ya kikazi badala ya barua ya kirafiki. Aidha mtahiniwa huyu hakuzingatia kanuni zote za barua za kikazi na hasa kanuni za uandishi wa mwisho wa barua.

Watahiniwa wengine waliandika muundo wa kadi ya mwaliko badala ya barua ya kirafiki. Kielelezo 8.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetumia sehemu ya swali kama jibu.

**Kielelezo 8.3**



Kielelezo 8.3 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kabisa kujibu swali kwa kuzingatia vipengele vya uandishi wa barua ya kirafiki. Aidha, hakufuata taratibu za uandishi wa barua na lugha sanifu.

### *2.3.2 Swali la 9: Uandishi wa Insha*

Swali hili lililenga kupima uelewa, ubunifu na maarifa ya uandishi wa insha. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika insha ya maneno yasiyopungua mia mbili hamsini (250) na yasiyozidi mia tatu (300) kuhusu umuhimu wa huduma za simu ya mkononi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10 na lilijibiwa na asilimia 30.6 tu ya watahiniwa wote waliofanya mtihani ambapo asilimia 66.6 walipata chini ya alama 5.

Asilimia 4.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata alama 0. Watahiniwa hawa hawakuzingatia matakwa ya swali kwani badala ya kuandika umuhimu wa simu waliandika umuhimu wa mazingira kama misitu, siku ya ukimwi na watoto wa Afrika. Kielelezo 9.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambayo hayakuwa sahihi.

**Kielelezo 9.1**


9 Insha

WATOTO WA AFRIKA

Watoto wa Afrika ni kundi moja
wapo katika jamii za kiafrika
linalo stahili kupewa haki zam
sing haki zao za msingi ni kama
ifuatavyo
Malezi bora watoto kama wa
toto wana stahili kupewa male
zi bora na wazazi wao ili kuepu
kana na majanga mbalimbali kama
vile uvutaji wa bangi
Elimu watoto lazima wapew
e haki yao katika suala la elimu

Kielelezo 9.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye hakujibu swali kwa usahihi. Mtahiniwa alitunga kichwa chake cha insha “Watoto wa Afrika” na hivyo kujibu kinyume na maelekezo ya swali.

Watahiniwa wachache sana (5.9%) kati ya watahiniwa wote waliofanya swali hili ndiyo waliopata kati ya alama 7 hadi 9, kwa kuwa waliweza kuandika kwa undani umuhimu wa matumizi ya simu za mkononi, kwa kufuata taratibu za uandishi wa insha. Kielelezo 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili.

**Kielelezo 9.2**

9. UMUHIMU WA HUDUMA ZA SIMU YA MKONONI.

Simu za mkononi zimekuwa ni kitu muhimu sana kwa wananchi. Wafanyabiashara, viongozi wa serikali, wafanyakazi, wote wana simu za mkononi kwasababu husaidia katika mambo mbali-mbali. Umuhimu wa huduma za simu za mkononi ni;

Huokoa muda. Kupitia simu za mkononi, watu wanaweza wakapeana ujumbe bila kukutana ana kwa ana ambapo shughuli nyingine zote zinakuwa zimesimama (haziendelei). Simu za mkononi huwawezesha watu kuongea, hata kuonana uso kwa uso katika simu zilizo-tengenezwa na teknolojia mpya.

Hurahisisha mawasiliano. Watu wanaweza kupeana taarifa kwa kifupi kupitia simu za mkononi. Ujumbe mfupi unaweza kuandikwa kwenye simu na kupitia mtandao, utamfikia mlengwa wa ujumbe huo.

Simu za mkononi hurahisisha upatikanaji wa mahitaji mbalimbali ya nyumbani kama umeme na maji. Kupitia simu za mkonono, watu wanaweza kulipia maji na umeme hata kuagiza vitu kwa kutumia simu. Hivyo hurahisisha upatikanaji wa mahitaji muhimu ya nyumbani, hata ada zinalipwa kwa kutumia simu.

Watu wanaweza kupata mikopo kwa kutu-mia simu. Hata mtu mmoja anaweza kutuma pesa kwa mwingine kupitia M-Pesa kwenye mtandao wa Vodacom au hata Tigo Pesa.

Kielelezo 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

## 2.4 Maendeleo ya Kiswahili

### *2.4.1 Swali la 10: Maendeleo ya Kiswahili*

Swali limetoka kwenye mada ya Maendeleo ya Kiswahili. Swali lililenga kupima maarifa na utumizi. Swali lilimtaka mtahiniwa afafanue jinsi shughuli za dini, utawala, biashara na elimu zinavyokuza na kueneza Kiswahili nchini. Swali hili ambalo lilikuwa na jumla ya alama 10 lilijibiwa na asilimia 85.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani ambapo asilimia 80.5 walipata chini ya alama 5.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya kwani asilimia 51 ya watahiniwa waliofanya mtihani walipata alama 0. Watahiniwa hawa walifafanua hoja kwa kurejea kipindi cha ukoloni na si kipindi cha sasa kama swali linavyotaka. Baadhi ya watahiniwa hao wamejibu bila kuanza na utangulizi na wengine walitoa utangulizi na hitimisho lisilohusiana na swali. Aidha watahiniwa hawa walitoa hoja ambazo hazihusiani na ueneaji na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Kielelezo 10.1 kinaonesha majibu ya watahiniwa wa aina hiyo.

**Kielelezo 10.1**

10 Shughuli za Dini, Biashara, utawala na Elim
zinavyo kuza na kueneza lugha ya kiswahili
uchini Tanzania
Biashara: Hii ni aina ya biashara ambayo
humfanya mtu aweze kutwamua maisha ya
baadaye
Dini: Hii ni aina ambayo mtu ni lazima
awe nayo kwani dini ni msingi kwa maish
Elimu: Hii ni lazima kwani mtu akiwa
hana elimu basi hana maisha mazuri ya
kuishi
Utawala: Hii ni sehemu ya kutawaliwa
na watu wa makabila mengine mfano:
Wazungu wakiondoka kwao uzunguni na kuja
Tanzania na kuleta lugha yao ya kizungu
ambacho ni (Kiingereza).

Kielelezo 10.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa kigezo cha wakati kwa kujibu swali hili kwa wakati uliopita (kipindi cha ukoloni) badala ya wakati wa sasa.

Watahiniwa wachache (10.3%) miongoni mwa watahiniwa wote waliojibu swali hili walipata alama kati ya 6 hadi 10. Katika majibu yao, watahiniwa hawa waliweza kufafanua jinsi dini, utawala, biashara na elimu zinavyokuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania na walitoa mifano ya maneno yanayopatikana kulingana na shughuli husika. Kielelezo 10.2 kinaonesha sampuli ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 10.2**

SEHEMU D.

10\. Kuenea kwa lugha ni namna lugha inavyopata watumiaji wengi zaidi na Kukua kwa lugha ni jinsi lugha inavyoendelea kupokea misamiati mipya hivyo kuikuza lugha husika. Lugha ya Kiswahili nchini Tanzania inakua na kuongezeka kwa kasi kutokana na shughuli mbalimbali kama ifuatavyo.

Dini. Katika kuhubiri au kutoa mawaidha misikitini au makanisani lugha ya Kiswahili inaendelea. Kwa mfano katika mahubiri ya Kikristo huhudhuriwa na watu wengi hivyo Kiswahili kinazidi kuenea hata wahubiri husafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine kuhubiri nako pia kuna eneza kiswahili. Hivyo hivyo pia katika dini ya kiislamu utoaji mawaidha ni kwa njia ya kiswahili na mahubiri yote hufanyika kwa lugha ya kiswahili. Misamiati inayotokana na mahubiri ya kidini ni kama kuruani, katekisimu, rozali na sakramenti.

Utawala. Shughuli za kiutawala nchini Tanzania zinatendeka kwa kutumia lugha kuu ya Taifa yaani Kiswahili. Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huhutubia nchi kwa njia ya lugha ya kiswahili. Pia katika bunge majadiliano yote hufanywa kwa lugha kiswahili.

Kielelezo 10.2 kinaonesha sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyefafanua shughuli za kidini na utawala zinavyoweza kukuza na kueneza lugha kwa kutoa mifano mbalimbali kama vile matumizi ya maneno kama kuruani, katekisimu

## 2.5 Sehemu E: Fasihi kwa Ujumla

### *2.5.1 Swali la 11:Fasihi Simulizi*

Swali hili lilitoka katika mada ya Fasihi simulizi na lililenga kupima maarifa, uundaji, udadisi na tathmini. Swali hili lilikuwa na alama 15 na liliwataka watahiniwa watumie methali sita (6) za Kiswahili ili kudhihirisha kuwa matumizi ya methali yasipozingatia muktadha yanaweza kuleta madhara kwa jamii.

Watahiniwa wachache sana (25.2%) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani ndiyo waliojibu swali hili. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 56.8 walipata chini ya alama 6. Watahiniwa hao walishindwa kabisa kuelewa haja ya swali, badala yake waliandika mambo tofauti yasiyohusiana na maelekezo ya swali. Aidha, baadhi yao walitaja vitendawili na wengine walisimulia hadithi. Mfano, mtahiniwa mmoja alijibu swali hili kama ifuatavyo:

*(i) Nyumba yangu ndogo watu wengi*
*(ii) Nampiga mwanangu nalia mwenyewe.*
*(iii) Athumani mfupi yupo mlangoni*
*(iv) Uku zii na uku ziii*
*(v) Nyumba yangu ina mlango juu*
*(vi) Nyumba yangu haina mlango*

Asilimia 3.7 tu, miongoni mwa watahiniwa waliofanya swali hili waliweza kupata alama kati ya 10 – 15. Kielelezo 11.1 kinaonesha sampuli ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 11.1**

11) Methali ni moja ya kipengele cha Semi kutoka katika fasihi simulizi kinachoelezaa mambo yaliyo katika jamii kwa uhalisia na kufundisha. Watu wengi hutumia methali kama chombo cha kumkumbusha na kumrahihisha mtu. Ni kweli kuwa methali ikitumiwa vibaya ina weza kuleta madhara makubwa kwa jamii. kwa kuelezea methali zifuatazo na madhara yake.

Mgaagaa na upwa hali wali mkavu, ha pa methali hii inamaana kuwa mtu anayepende lea kushinda pembezoni mwa bahari lazima ata pata kitowea na kwenda nacho nyumbani kwa mlo. Hasara ya methali hii ni kwamba sio kila an ayeshinda Pembezone mwa bahari yaani upwa ana

weza kupata kitoweo. Hivyo watu wanapaswa kutotumia kigezo hiki na kutojibarisha ~~kufanya~~ kazi, ~~wa~~ kwani sio kila kitu mtu unasaidiwa na watu, unaweza ukafa kwa umasikini.

Mvumilivu hula mbivu, methali hii ina maana kuwa mtu anayevumilia hupata vitu ambavyo ni bora zaidi. Hasara ya methali hii ni kuwamba sio kila mtu anayevumilia hupata vitu vizuri unaweza ukaambulia vitu vibovu. Hivyo watu wasitumie kigezo cha methali hii kuvumilia mambo ambayo si ya msingi. Kwa mfano mtu anapokuwa ananyanyaswa anatakiwa kwenda ~~ku~~shitaki mahali husika na sio kuvumilia kwani badala yake anaweza akaambulia kifo.

Yote yang'aayo usidhani dhahabu, methali hii inamaana kuwa sio kitu kinachoonekana kwa umbo la nje ukadhani ndio chema, kwani kuna vitu vingine au watu ni watakatifu wa usoni lakini moyoni ni waovu ni sio kuwavamia ghafla. Hasara ya kutumia methali hii ni kuwamba kuna watu au vitu vingine ni vizuri kwa nje na moyoni mwao pia wakawa na wazuri. Hivyo mtu asitumie kigezo hiki kutokuomba msaada kwa watu watanashati au wazuri kwa kudhani kuwa ni wabaya hivyo inabidi kuwa makini kutokana na hali halisi ya maisha inavyokuwa

Pole pole ndio mwendo, methali hii ina maana kuwa watu wanapotaka kufanya kitu lazima wawe taratibu ndipo wanaweza ~~kutumia~~ kupata mafanikio bila kutumia papara. Hasara ya methali hii ni kuwamba sio kuwamba

11 Kila hitaji au lengo la mtu ni lazima litayani
kiwa kwa kwa kuwa polepole. lazima mtu ki
fanye haraka ili iweze kupata unachokitaka. Hiv
yo matumizi ya methali hii kwa upande mwi
ingine yana hasara.

La kuvunda halina ubani, methali hii
ina maana kuwa kitu chochote kilichoharibika ha
kiweza kurudia tena katika hali yake kama
mwanzo. hata kwa kutumia ubani au marashi.
Hasara ya methali hii ni kwamba sio vyote
vinavyoharibika haviwezi kutengenezeka, kuna vitu
vingine viraweza kutengenezeka na kurudi katika
hali yake. Hivyo watu wanapaswa kuwa makini
na methali hii katika matumizi hurika.

Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu, methali
hii ina maana kuwa mtu asiyesikia jambo an
alohuriwa na mkubwa anaweza kupata madhara
baadaye. Utumiaji wa methali hii unahasara
kwani kunabaadhi ya wakubwa huwafundisha
watu tambaa mbaya na wao huiga kutoka kw
ao, hivyo si kila linalotoka kwa mkuu ni la m
uhimu. Methali hii inapaswa kutumiwa kwa u
makini wa hali ya juu.

Hitimisho, methali ni moja ya
chombo kinachotoa ujumbe kwa jamii kiwani
methali zote hueleza na kuonya jamii kuhu
su matokea ya baadaye yanayoweza kuto
kea baada ya kufanya jambo fulani. Hivyo
jamii inapaswa kuwa makini na utumiaji wa
methali kwani zinafaida na hasara zake.

Kielelezo 11.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua methali nne ambazo zinadhihirisha kuleta madhara kama muktadha wa methali hizo hautazingatiwa, hata hivyo alikosa alama 01 kwa kuwa alishindwa kuelezea vizuri maana ya methali aliyoitoa katika kipengele cha (i) “ Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.”

### *2.5.2* Swali la 12: Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya Fasihi Andishi na lilihusu vitabu teule vya ushairi ambapo lililenga kupima maarifa, uchambuzi, ulinganifu na tathimini. Swali liliwataka watahiniwa kutumia diwani mbili walizosoma kuonesha jinsi taswira tatu kutoka katika kila kitabu zinavyoweza kutoa ujumbe katika jamii. Swali hili lilikuwa na alama 15 na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na watahiniwa wachache sana (21.5%) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani.

Asilimia 26.2 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama 0. Baadhi ya watahiniwa hawa hawakuelewa maana ya diwani kuwa ni kitabu chenye mkusanyiko wa mashairi hasa ya mtu mmoja na badala yake walitumia diwani kama kiongozi wa kisiasa kwa ngazi ya kata, hivyo kutoka nje ya maelekezo ya swali kwa vile walikosa maarifa yaliyohitajika. Vilevile miongoni mwa watahiniwa hao, walichanganya maelezo ya vitabu tofauti yaani ushairi, tamthiliya na riwaya. Aidha baadhi ya watahiniwa hao katika uchambuzi wao walijadili dhamira badala ya taswira. Pia kanuni za uandishi wa insha hazikufuatwa pamoja na matumizi ya vituo na herufi kubwa hasa yanapotajwa majina ya pekee kama majina ya vitabu "Wasakatonge", "Malenga Wapya" na jina la mwandishi M.S. Khatib. Kielelezo 12.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa ambaye alijadili dhamira kinyume na haja ya swali, hakufuata kanuni ya uandishi na matumizi ya vituo.

**Kielelezo 12.1**

12. Umetumia diwani ya wasakatonge ambayo imeandikwa na M.S. Khatibu pamoja na malenga wapya. ambapo dhamira kubwa katika wasakatonge ni ukombozi maana tunawaona jinsi watu wanavyo nyanyasi-ka baadhi ya watu wano nyanyasikani walalahoi, wavuja jasho wenye wa tabaka la chini.

Zifuatazo ni sababu zinazo onyesha kuthibitisha kuwa hii katika shairi la wasakatonge.

Nafasi ya mwanamke katika jamii mwanamke amechorwa katika nafasi mbali mbali kama zifuatazo amechorwa kama chombo cha starehe hii tunaona katika shairi la "Nilikesha" uk 21 "Mahaba" uk 1 vilevile mwanamke amechorwa kama chombo finyu asiye penda maendeleo hii imezungumuziwa katika shairi la "Madkitetu" uk 21 "Unyama" uk 41

Kupiga vita uongozi mbaya hii katika diwani ya wasakatonge imezungumuziwa katika baadhi ya mashairi kama vile "Unyama" uk (47-48) Madkitetu uk 21

Kupiga vita ukoloni mwambo leo hii katika diwani ya wasakatonge imeweza kuzungumziwa katika baadhi ya mashairi "Samaki mtunaoni" uk 51

Kielelezo 12.1 ni jibu ya mtahiniwa ambalo sio sahihi kwa vile alieleza kuhusu dhamira badala ya kufafanua taswira na kuonesha jinsi zinavyofikisha ujumbe kwa jamii.

Asilimia 14.4 ya watahiniwa walipata kati ya alama 10 hadi 15. Watahiniwa hawa walikuwa na utangulizi mzuri ulioendana na swali. Aidha watahiniwa hawa walifafanua hoja na kutoa hitimisho lililoendana na swali, kwa kuzifafanua taswira mbalimbali na kuonesha jinsi zinavyofikisha ujumbe kwa jamii. Kielelezo 12.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa lililokidhi haja ya swali kwa kutoa taswira mbalimbali na kuonesha jinsi zinavyofikisha ujumbe kwa jamii.

## Kielelezo 12.2

wanaume ambao hawatoi hela ya mahari kwa wapenzi wao hivyo mwandishi na msanii ~~ana~~ amewahusia wache mambo kama hayo.

"Malenga Wapya", msanii ametumia picha ya "Ua" katika shairi la "Ua" kuonyesha kwamba mapenzi ya dhati yanatakiwa yawepo katika jamii yetu ili jamii isonge mbele kimaendeleo.

Pia msanii ametumia taswira ya "Punda" katika shairi la "Punda" akimaanisha watu wa ~~tabaka~~ tabaka la chini ambao wanabebeshwa mizigo mbalimbali katika jamii lakini hawaifaidi matunda ya mizigo hiyo. Hata katika jamii kuna hali kama hiyo hiyo mwandishi ameieleza hali hiyo.

Si tu taswira hizo bali taswira ya "Samaki" akimaanisha watu wa tabaka la chini katika shairi la "Samaki Mtungoni" na mvuvi akiwa ndiyo tabaka la juu ambaye ni kiongozi mbaya asiyetakiwa kuigwa na jamii yetu.

Kwahiyo, wasanii wamekuwa watetezi wazuri na walio bobea katika kutumia taswira kwani wameitumia kutoa ujumbe mbalimbali katika jamii na hivyo kusaidia katika kukomboa jamii kimaadili, kifikra na kisiasa.

Kielelezo 12.2 kinafafanua sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali la 12 kwa kufafanua taswira kama vile "ua", "punda" na "samaki" zilivyotumika kufikisha ujumbe kwa jamii.

### *2.5.3 Swali la 13: Riwaya*

Swali hili lilitoka katika mada ya fasihi andishi hasa kuhusu vitabu teule vya riwaya na lililenga kupima maarifa, uchambuzi pamoja na tathmini. Swali hili liliwataka watahiniwa kutoa hoja tatu (3) kutoka katika riwaya mbili walizosoma ili kuthibitisha kuwa mwanaume ni kikwazo cha mafanikio katika jamii. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15 na lilijibiwa na asilimia 49.3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani ambapo kati yao, asilimia 51.2 walipata chini ya alama 6 na miongoni mwao asilimia 13.6 walipata alama 0. Watahiniwa hawa hawakuwa na hoja sahihi zilizojibu swali kwani baadhi yao walijikita katika kumwelezea mwanamke kuwa ni/si kikwazo cha maendeleo katika jamii badala ya kumwelezea mwanaume kuwa kikwazo kama swali lilivyokuwa linataka. Kielelezo 13.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeelezea kuwa mwanamke si kikwazo tofauti na matakwa ya swali.

**Kielelezo 13.1**

13. Mwanamke ni kikwazo cha mafaniki-
kio katika jamii. Nakanusha kauli hii
kwa kutumia k riwaya ya TAKADINI iliyo
andikwa na Ben Hanson pamoja na riwa
ya ya WATOTO WA MAMANTILIE iliyo andi
kwa na E. Mbogo.

Kwa kuanzo na kitabu cho Takadi
ni Mwanamke sikikwazo cha mafanikio
katika jamii kwa sababu.

Mwanamke ni mlezi katiko familia
katika hii riwaya tunaona mwandishi ali
yyo mchoru mwanamke ambaye ni Sekai.
Sekai ~~atiku~~ alimpa mwanaye Takadini
malezi mazuri japokuwa alikuwa ~~hatha~~ hatha-
miniwa na watu kutokana na kuwa
mlemavu. Hapa tunaona kabisa kuwa Se-
kai ni chanzo cha mafanikio katika
kujenga jamii.

Mwanamke ni jasiri. Pia tena Mwa
na mke huyu Sekai alipoona kuwa
jamii yote inataka kumuua Takadini
kutokana na kuwa zeruzeru alijitoa
muhanga akasema atamlea mtoto wake
Takadini mpaka siku ya kufa na kua
mua kutoroka naye. Hakujari huko
njiani kakaa kuna wanyama wakali
Ndio maana tunasema Mwanamke ni
chanzo cha mafanikio.

Mwanamke ana Mapenzi ya dhati
Mwanamke ambaye ni Sekai tunaona
kuwa alikuwa na juhudi katika kumfa

riji wanayo pale alipokuwa akimwona mwanaye akihurumika kwasababu watu katika jamii hawamthamini. Kutokana na hali hii ilipelekea, mudo kipindi ambacho Takadini alipokuwa mtu mzima watu wakamzoea na kuona kama naye ni mtu kama wengine.

Kwa kutumia riwaya ya Watoto wa mamantilie. Mwanamke ni daraja la mafanikio katika jamii kwa sababu:

Mwanamke ni mchapakazi. Hapa tunamuona mhusika Mama Zita alipo kuwa akifanya biashara yake kule gengeni ili watoto wake wasome pia na kulea familia. Kutokana na hali hi inaonesha wazi kuwa mwanamke ni daraja la mafanikio katika jamii

Mwanamke ni mwenye huruma. Hapa pia tunamuona mhusika Zainabu aliyokuwa akiwahurumia watoto wa mamantilie na kuwapa chakula. Kwa hiyo tunatambua kuwa Zainabu alikuwa amesaidia kupunguza mzigo mkubwa wa kuwalea watoto wa mamantilie.

Mwanamke ni mlezi na ni mvumilivu. Mhusika Mamantilie alikuwa akivumilia kumtunza Mzee lomolomo pamoja na kuwalea watoto wake peter na Zita. Kwahiyo mwanamke sikikuwaro katika kulea ma-


13. Fanikio katika jamii.
Mwisho kabisa napenda kusema
kuwa Mwanamke ni mkombo wa kiute
maduni na pia ni muhimu katika
jamii kwa sababu ni chanzo daraja
la maendeleo.

Kielelezo 13.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetumia nafasi ya mwanamke kuonesha kuwa sio kikwazo badala ya kutumia nafasi ya mwanaume kama kikwazo cha mafanikio katika jamii.

Asilimia ndogo (11.2) ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata kati ya alama 10 hadi 14. Kwa kiasi kikubwa watahiniwa hawa walizingatia haja ya swali na waliweza kuwataja wahusika waliosadifu wanaume kuwa ni kikwazo cha mafanikio katika jamii. Kielelezo 13.2 kinaonesha sampuli jibu la mtahiniwa lililojibiwa vizuri.

**Kielelezo 13.2**

13 Kwa kutumia riwaya mbili nilizosoma, ambazo ni WATOTO WA MAMA NTILIE iliyoandikwa na E. Mbogo (H.P) na JOKA LA MDIMU iliyoandikwa na A.J. Safari (H.P) nitathibitisha kuwa mwanaume ndiye kikwazo cha maafanikio katika jamii.

MAMA NTILIE: Ulevi ulioonesbwa na mzee Lomolomo. Mzee Lomolomo alikuwa baba asiyejali familia yake. Alikuwa akishinda kilabuni akilewa pombe. Hakujali familia yake hata kidogo. Ulevi wake ulikwamisha maendeleo ya watoto na mke wake, kwani Mama ntilie ndiye aliyebakiwa na jukumu la kuwasomesha pamoja na kuwalisha watoto wake. Jambo hili lilimuongezea mama ntilie majukumu na kumnyima ashindwe kuendeleza na shughuli nyingine za kimaendeleo.

Ujambazi ulioonesbwa na Dani pamoja na Doto: Dani na Doto ni wanaume waliokosa elimu na kazi. Hawakuwa na wazazi wala mlezi. Hivyo shughuli walioiona inafaa kwao ni wizi na ujambazi. Waliiba katika sehemu mbalimbali. Ujambazi wao ulikwamisha maendeleo ya wengine. Kwani kipato ambacho wamekiiba kingetumika kuendeleza shughuli nyingine za kujenga taifa.

Biashara za madawa ya kulevya zilizoonesbwa na Peter pamoja na Musa: Musa alikuwa kijana asiyependa shule na ambae hakujali familia yake husussani mama yake mzazi. Alipenda kuishi peke yake ili asisumbuliwe na afanye shughuli zake bila usumbufu. Peter alikuwa na familia ambayo aliipenda sana. Kuachana na mapenzi yake na familia yake pia alipenda sana shule. Hii ndio sababu iliyomfanya ajihusishe na biashara za kuuza madawa

ya kulevya. Alihitaji pesa za kumrudisha shuleni kwani alifukuzwa kwa ajili ya ada na kukosa sare za shule. Hivyo basi kukuza kwao kwa madawa kulikuwamisha maendeleo ya jamii kwani vijana wengi huacha kwenda shule na kujihusisha na madawa hayo.

JOKA LA MDIMU; Ujangili uliooneshwa na Brown Kwacha: Brown Kwacha alikuwa mwanaume kiongozi ambae alitumia vibaya mali ya umma. Alitumia mali ya umma kwa manufaa yake mwenyewe. Mfano Brown Kwacha aliiba ndovu za tembo na kuziuza/firisha nje kiholela na kudai zimepotea. Ndovu hizi zingetumiwa katika kukuza uchumi wa jamii hivyo amekuwa chanzo cha kukwaza mafanikio katika jamii.

Wizi na ujambazi ulioonekana na Tino pamoja na Amani: Amani alikuwa rafiki mwandani wa Tino. Yeye ndiye aliyemshawishi Tino akaibe benkini kupata pesa za kumpeleka Cheche hospitali ulaya. Amani alichangia usafiri na vifaa (bastola) ya kuibia. Pesa walizoiba katika benki zingesaidia kukuza uchumi wa jamii.

Ufisadi ulioonekana na Brown Kwacha: Brown Kwacha kiongozi katika serikali alitumia mali ya umma kwa manufaa yake. Alitumia pesa hizo kujenga nyumba mbili za kifahari. Pia alizitumia kwa wanawake wake (hawara) kama Leyla. Ufisadi wake ulikwamisha maendeleo ya jamii kwani meli iliyokuwa imeleta mafuta ilirudi bila kushusha mzigo kwani pesa ambayo alitakiwa kutoa kwa ajili ya mafuta ilikosekana hivyo kuacha jamii na tatizo la mafuta.


Wasanii wa riwaya zote mbili "MAMA NTILIE" na "JOKA LA MDIMU" wamefanikiwa kuonesha jinsi wanaume wanavyochangia kwa kikwazo cha mafanikio katika jamii kwa kuwa walevi na kutoa jali familia, kujihusisha na madawa ya kulevya, ujambazi, ufisadi, ujangili na wizi. Pia wamefanikiwa kuelimisha jamii kwani katika jamii yetu kuna wanaume kama hawa wanaokwaza maendeleo ya jamii

Kielelezo 13.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyekuwa na utangulizi mzuri ulioendana na swali, hoja zenye ufafanuzi na kutoa hitimisho linaloendana na swali, kwa kuwataja wahusika waliosadifu wanaume kuwa ni kikwazo cha mafanikio katika jamii.

### *2.5.4 Swai la 14: Tamthiliya*

Swali la 14 lilikuwa ni la Fasihi Andishi katika kipengele cha Tamthiliya. Swali lililenga kupima maarifa, uchambuzi, udadisi pamoja na tathmini. Swali liliwataka watahiniwa watoe hoja tatu (3) kwa kila kitabu katika tamthiliya mbili zilizoorodheshwa ili kujadili madhara ya ukosefu wa elimu katika jamii. Swali hili lilikuwa na alama 15 na lilijibiwa na asilimia 72 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani, miongoni mwao asilimia 35.1 walipata chini ya alama 6 kwani walishindwa kukidhi matakwa ya swali. Baadhi yao walijadili kuhusu dhamira mbalimbali zinazotokana na tamthiliya hizo badala ya kueleza madhara yanayotokana na ukosefu wa elimu kama swali lilivyoulizwa.

Kielelezo 14.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hilo kwa kujadili dhamira mbalimbali kinyume na haja ya swali.

**Kielelezo 14.1**

14 Swali limejibiwa kwa kutumia tamthilia ya Ngoswe penzi kitovu cha uzembe.

Ngoswe Penzi kitovu cha uzembe ni tamthilia iliyo andikwa na E. Semzaba (ESC)

Katika tamthilia ya Ngoswe penzi

14 kitovu uzembe ni tamthilia ambayo imethibitishwa jamii kwa ujumla kama tulivyo ambiwa kwamba Ngoswe ni kijana mdogo ni kijana ambaye alikuwa muelewa sana katika kijiji chao. Katika kijiji cha Ngoswe kuli kuwa na kazi ya usahabuji watu kazi ~~hiyo~~ hiyo alipewa Ngoswe ambaye yeye alikuwa mtu muaminifu Ngoswe alikuwa baadaye muhesabuji watu katika kijiji chao.

Dhamira kuu katika tamthilia hii ni Suala la umasikini Ngoswe ni kijana ambaye alikuwa kuinua maisha ya kijiji chao pia hata kwenye familia yao lakini Ngoswe alikuwa akifanya kazi ya muesabuji watu huku akiongozana na baba ye mee mito mingi Ngoswe akaamua kuacha kazi kwa sababu aliona mee mitomingi anakula sana mali za Ngoswe hadhafu mee mitomingo hata ~~na~~ kamjali.

Suala la mapenzi Ngoswe alikuwa kijana ambaye mtulivu sana katika kijiji chao ila ~~tu~~ kitu kilicho msababisha Ngoswe ~~kuacha~~ kutamani mapenzi ni wakati mwanzi bado mdogo Ngoswe kuja kuja kumwita mazoea na kutoroshwa huku mee mito mingi kuwa na adhari ~~kwa~~ kwa Ngoswe Ngoswe alikuwa mfisa muhesabuji watu sasa kutamani mapenzi huku akiwa na mwanzi mdogo.


14 Suala la uvivu katika dhamira ya ngoswe
kitovu cha uzembe ni dhamira ambayo
imekithiri Tena la suala uvivu katika
jamii si nzuri kwani unakandamiza maisha
unyonge na kuwa na hali mbaya zaidi
katika jamii inapinga juu ya suala ya
uvivu lisiwepo katika jamii

Kielelezo 14.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kuhusu dhamira badala ya kueleza madhara ya ukosefu wa elimu.

Asilimia 13.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 10 hadi 14 kati ya alama 15. Watahiniwa hawa walijitahidi kuzingatia matakwa ya swali kwa kutoa hoja zinazohusu madhara ya ukosefu wa elimu kama vile vifo vinavyotokea kutokana na jamii kukosa elimu kwa mfano athari zitokanazo na ugonjwa hatari wa UKIMWI, kuwepo pia kwa imani za kishirikina miongoni mwa wana jamii ambao waliiona sensa kama uchawi badala kuwa ni jambo jema la kuiletea jamii maendeleo.

Kielelezo 14.2 kinaonesha sampuli ya sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa kufafanua madhara mbalimbali yaliyotokana na ukosefu wa elimu.

**Kielelezo 14.2**

14 Elimu ni ujuzi unatolewa na watu kwenda kwa watu wengine ili wale wanaoupata huo ujuzi waweze kutumia mawazo na nafasi ~~z~~ zao vyema. Elimu isipokuwepo katika jamii athari kubwa hujitokeza kama vile: vurugu na hata umaskini katika tamthilia hizi mbili ambazo ni kilio chetu na Ngoswe penzi kitovu cha uzembe kuna madhara mengi yaliojitokeza ~~kulingana~~ kutokana na ukosefu wa elimu.

Kwa kuanza na kilio chetu kuna madhara kama mimba za utotoni, hii ilimtokea Suzy ambapo alipata mimba akiwa darasa la tano ambayo alipewa na mwanafunzi mwenzake Joti. Haya yote ~~yalim~~ yalimtokea pale ambapo alikosa elimu ya jinsia juu ya kujihusisha na mapenzi katika umri mdogo ambapo alikosa hiyo elimu kutokana na mama yake kutomwambia kitu. Hivyo basi jamii itaweza ~~kudhibika~~ kuathiriko na tatizo hili endapo itaamua kutoa elimu kwa vijana juu ya madhara ya mapenzi katika umri mdogo.

Hata hivyo kuna athari za magonjwa hatari ya Ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa. Katika ~~Magonjo~~ kitabu tunaonyeshwa Joti ambaye aliathirika na ugonjwa wa Ukimwi kwa sababu ya kukosa elimu juu ya huo ugonjwa yaani jinsi unavyo-ambukizwa na jinsi ya kujikinga. Alikuwa akitembea na wanawake wengi mfano Suzy na Chausiku. Ukosefu wa elimu ulimfanya akapata Ukimwi. Hivyo basi elimu ni muhimu kwa jamii kwani isipotoa elimu juu ya Ukimwi basi vijana watakufa na hivyo kupunguza nguvu kazi ya jamii na ukuaji wa taifa

14 Pia kuna athari ya kifo katika jamii, kwani Joti alifariki kwa kukosa malezi bora kwa mgonjwa wa UKIMWI. Wazazi wake waliamini kuwa amelogwa na walitaka kumpeleka kwa mganga. Hata hivyo alikuja kushauriwa na mjomba baadaye ambapo Joti alikuwa keshakufa. Hivyo athari ya kutopata elimu ya malezi sahihi kwa mgonjwa wa ukimwi inasababisha vifo vya vijana katika jamii.

Katika tamthilia ya Ngoswe penzi kitovu cha uzembe madhara ya kutopata elimu ni kama vile kusababisha kazi ya uhesabuji wa watu kukwama. Hapa Ngoswe alivyoenda kuhesabu watu wa huko kijijini walikuwa hawajaelimika kwani walikuwa hawajui ni maana ya kuhesabu watu na umuhimu wake hivyo, wengine walipuuzia na kwenda kunywa pombe na wengine wakaona kuwa ni kama uchawi fulani hivyo Ngoswe akashindwa kupata hesabu ya watu. Hivyo basi vijijini wanatakiwa kupewa elimu kwanza kabla ya kuwaonyesha vitu vipya ambavyo hawajawahi kukutana navyo.

Athari nyingine ni kusababisha vifo vya watu. Hapa tunaona kijiji cha Balozi Mitomingi hapakuwa na hospitali karibu na kutokana na watu kukosa elimu mtu akiugua kidogo walijua amelogwa. Kama mama ambae mumewe alikufa, alidai kuwa mume wake alikufa akiwa na nguvu zake na hivyo alilogwa. Ila hakidhubutu kumpeleka mumewe hospitali kutibiwa. Hivyo ukosefu wa elimu kwa mkewe kulisababisha mume afe kwa ugonjwa ambao ungeweza kuzuhilika. Hivyo basi katika jamii kuna watu


kutokani na athari hapo juu za jamii kuto-
pata elimu. Jamii inatakiwa kujifunza kutokana na
athari. hizo hiyyo ~~kufanya~~ kuhakikisha kila mtu
katika jamii ana elimu kuhusiana na maisha kwa
ujumla ili asifanye kosa maishani litakalomgharimu
hata maisha yake. au heshima yake.

Kielelezo 14.2 kinaonesha sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua madhara mbalimbali yaliyotokea katika jamii kutokana na ukosefu wa elimu.

### *2.5.5 Swali la 15: Fasihi Simulizi*

Swali hili linatoka katika mada ya Fasihi Simulizi na lililenga kupima maarifa, uchambuzi, uundaji na tathmini na liliwataka watahiniwa kuandika majigambo yenye beti nne (4) yanayohusu mwalimu, likiwa ni swali la lazima lenye jumla ya alama 15.

Asilimia 96.3 ya watahiniwa wote walijibu swali hili, ambapo asilimia 67.9 walipata alama 0. Watahiniwa hawa waliandika mambo mengine mbalimbali kama dayalojia, mashairi na tenzi badala ya majigambo. Kielelezo 15.1 kinaonesha sampuli ya mtahiniwa ambaye aliandika dayalojia badala ya majigambo.

**Kielelezo15.1**

SANAA YA MAONESHO.

15

Mwalimu: Hodi

15'

1 Mgeni: Habari ya ~~ba~~ leo ndugu Mwalimu

Mwalimu: Nzuri tu za kwako je?

Mgeni: Nzuri tu na pia ni vyema

Mwalimu: Karibu sana. katika siku hii ya leo

2 Mgeni: Absante sana.

Mwalimu: Kama unavyoona siku imepambwa motomoto

Mgeni: hata mimi naona ni inapendeza sana

Mwalimu: Kama unavyofahamu ni jinsi gani sisi walimu ~~tuliyo~~ tulivyokuwa Muhimu sana katika jamii

3 Mgeni: Ni kweli kabisa Mwalimu unayosema ni kweli

Mwalimu: Kwa sababu bila sasa tusingekuwa na madaktari

Mgeni: Nakubali kabisa bila ya Hate shaka

Mwalimu: Sisi tunawaenzi watu wowe na kazi nzuri

4 Mgeni: Yote hayo ni ya kweli ~~k~~ kabisa

Mwalimu: Siku hii ni muhimu sana kwetu kusherekea

Mgeni: Inabidi Serikali iwajali sana kwa hali na mali

Mwalimu: kweli ~~t~~ natubaliana na hilo hii ikijumuisha kutupatia mishahara nyongeza na marupurupu kwa sana kwa jinsi ~~tunavyokaa~~ tunavyofanya kazi kwa bidii na kiumakini sana

Kielelezo 15.1 kinachoonesha majibu ya mtahiniwa ambayo hayakukidhi haja ya swali. Mtahiniwa ameandika dayalojia badala ya majigambo.

Aidha katika swali hili baadhi ya watahiniwa katika kituo kimoja walikuwa na utunzi wa majigambo uliokuwa na mfanano usio wa kawaida kwani wote waliandika kama ifuatavyo: *“Mwalimu! mwalimu! mwalimu!, mimi ni kioo cha jamii, bila mimi hujawa msomi, hivyo nalazimika kupangiwa, siku yangu ya sherehe duniani, hakika mimi napendeka, kwa watu wote wakubwa kwa wadogo, hivyo* ***hacheni*** *mimi niitwe mwalimu.”*

Katika ubeti huo, pamoja na kwamba watahiniwa hao wote walikuwa na mfanano usio wa kawaida, mfanano huo ulibainika zaidi kwa jinsi wote walivyokosea kuandika neno “acheni” na kuandika “hacheni” jambo lililoonesha kuwa walikuwa na chanzo kimoja cha majibu.

Watahiniwa wachache sana (2.6%) miongoni mwa waliofanya swali hili walijibu vizuri na kupata alama kati ya 10 hadi 13. Watahiniwa hawa waliweza kuandika majigambo kwa kuchanganya nafsi kwa baadhi ya beti, kutumia lugha ya kishairi, pia walitumia alama na vituo kwa usahihi. Kielelezo 15.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 15.2**

SEHEMU E:

15. Majigambo ni ushairi ulio na urari wa mistari yenye sifa na kujitapa kwa yule anayesema au aliyetunga.

Jemedari ndio mimi,
Nishatinga kiwanjani,
Nasimama mbele bila hofu,
Ni mwenye nguvu najiamini,
Nyie nyote bila mimi si kitu,
Elimu ninayowapa ni tamu,
Heshima nipeni kabisa,
Askari kama mimi hakuna.

Mimi ni simba ninguurumaye,
Anayebisha aje mbele,
Napambana na hali duni,
Si kwa mikuki na sime,
Ni kwa ujuzi ulio juu,
Nawapa ujuzi huu na ninyi,
Muwe ngangari kama mimi,
Kupambana na umasikini,
Eti umasikini, umasikini?!
Wakati mwalimu jemedari nipo!
Hakuna kitu kama hicho!

Maisha hamna bila mimi,
Hilo nina wahakikishieni,
Mimi ndio uhai wa watoto wenu,
Kwa ujuzi ninao watemea,
Umasikini nauweka mbali,


15\. Hauna neno mbele yangu,
Kwani mimi ni ngangari,
Elimu yangu naiamini.

Saluti zitoeni kwangu kwa wingi,
Tegemeo lenu la maisha,
Ni mgumu zaidi ya kisiki,
Siangushwi na ujinga na umasikini,
Elimu ninayo na zaidi,
Ya kutetea wanyonge wasionayo,
Mambo yangu si mchezo,
Naokoa jamii nzima,
Bila mimi jamii nyakanyaka,
Mimi ni tegemeo la Taifa,
Walimu wajipongeze,
Jemedari wa taifa!!

Kielelezo 15.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kudhihirisha vipengele muhimu katika kuandika majigambo vilivyojikita katika lugha ya kisanaa kama vile “simba”, “mkuki”, “kisiki” n.k vitu vinavyofanya majigambo yake yawe na uhalisia uliotakiwa, hata hivyo mtahiniwa alipoteza alama 01 kwa kutoandika kichwa cha majigambo.

## 3.0 HITIMISHO

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili mwaka 2012 ni cha kuridhisha ukilinganisha na cha mwaka 2011. Hata hivyo, mtazamo wa jumla unaonesha kwamba jitihada kubwa bado inahitajika ili watahiniwa wengi waweza kufaulu somo hili hasa ikizingatiwa kuwa hii ni lugha ya Taifa ambayo kila mmoja wao alipaswa kujieleza kwa umahiri bila ya kikwazo chochote. Pamoja na kwamba kumekuwepo na changamoto mbalimbali katika ujifunzaji na ufundishaji wa somo hili kiwango cha ufaulu kwa somo hili kinahitajika kiwe cha juu zaidi.

Uchambuzi uliofanyika unaonesha kuwa watahiniwa walijibu vibaya maswali ya Sarufi na Utumizi wa Lugha, Maendeleo ya Kiswahili na Fasihi kwa Ujumla. Pia imebainika kuwa, katika mada ya Fasihi kwa Ujumla yenye maswali ya kuchagua, watahiniwa walifanya vibaya katika swali la ushairi lililochaguliwa na asilimia 21.5 tu ya watahiniwa, pia swali la 11 linalohusu fasihi simulizi lililochaguliwa na asilimia 25.2. Aidha swali la 13 lililojikita katika riwaya lililochaguliwa na asilimia 49.3 halikujibiwa vizuri. Swali la Tamthiliya pekee ndilo lililojibiwa vizuri na lilichaguliwa na asilimia kubwa (72%) ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Aidha, katika mada ya Uandishi ambayo ina maswali mawili, swali la 8 lililohusu uandishi wa barua lilijibiwa vizuri zaidi na lilichaguliwa na asilimia 59.3 ya watahiniwa wakati swali la 9 lililohusu utunzi wa insha lililochaguliwa na asilimia 30.6 tu ya watahiniwa halikujibiwa vizuri. Hali kadhalika, swali la 15 lililotoka katika mada ya Fasihi kwa Ujumla limejibiwa vibaya sana na asilimia kubwa (67.9%) ya watahiniwa. Uchambuzi uliofanyika unaonesha kuwa miongoni mwa watahiniwa kulikuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali pamoja na uwezo mdogo wa kujibu maswali ya fasihi. Aidha watahiniwa hao walikuwa hawana ujuzi wa kutosha katika mada ya Fasihi kwa Ujumla hasa katika vipengele vya fasihi simulizi, ushairi na riwaya. Mada ndogo ya utunzi wa kazi za fasihi ina changamoto kubwa kwa watahiniwa kwani miongoni mwao, asilimia kubwa (67.9%) walishindwa kutunga majigambo.

## 4.0 Mapendekezo

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili inapendekezwa kuwa:

(a) Walimu waweke mkazo katika ufundishaji/ujifunzaji wa mada za Sarufi na Utumizi wa Lugha, Fasihi kwa Ujumla hasa katika vipengele vya fasihi simulizi, ushairi na riwaya kwa kuhamasisha wanafunzi kusoma vitabu teule, pia ufundishaji wa vipengele vya fani katika kazi za fasihi utiliwe mkazo zaidi.

(b) Wanafunzi wahamasishwe kujihusisha katika mada ndogo ya utunzi wa kazi za kifasihi.

Ni matarajio ya Baraza la Mitihani kuwa taarifa hii itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu wa somo hili, kwa kuwa itakuwa changamoto kwa walimu na wanafunzi katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa mada za Sarufi, Utumizi wa Lugha pamoja na Fasihi simulizi, hasa ikizingatiwa kuwa lugha ya Kiswahili ni muhimu kwani ni sehemu ya utamaduni wa mtanzania.